HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RAMADHAN ABDALLA SHAABANI KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2008/2009

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora ya Mwaka wa Fedha 2008/2009.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima wa afya na kuweza kufika hapa kuendelea na shughuli hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Tunaomba Mwenyezi Mungu atuzidishie busara, hikima na atuongoze katika muelekeo mwema na mashirikiano ili tuweze kutimiza majukumu yetu vizuri zaidi.

3. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume kwa kazi kubwa anazozifanya katika kuhakikisha ustawi wa maisha ya Wazanzibari. Juhudi zake za kusimamia vizuri mipango ya kuimarisha huduma za jamii na za maendeleo ni ushahidi thabiti wa dhamira yake na ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujenga maisha bora kwa wananchi wake. Hatua ya Mheshimiwa Rais kuendelea kutoa umuhimu wa pekee kwa Utawala Bora kama nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo, usawa na umoja wa kitaifa ni changamoto kubwa kwetu katika kutimiza majukumu yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa kazi za kila siku za Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** aidha, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa uwajibikaji wako katika kusimamia shughuli za Baraza lako hili tukufu. Sambamba na hilo nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako kwa kuweza kuifanya kazi waliokabidhiwa na wananchi katika majimbo yao. Pia nawapongeza na kuwashukuru wajumbe waliochangia hotuba ya Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2007/2008 na wajumbe wote wa Bazara lako kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kuleta maendeleo kwa wananchi wote.

6. **Mheshimiwa Spika,** pongezi na shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haji Omar Kheri kwa ushauri, maelekezo na busara zao wakati wote. Kamati hii imekuwa karibu sana na Wizara yangu na kwa hakika maelekezo ya kamati yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

7. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa uniruhusu kuelezea kwa muhtasari hali halisi ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

UTEKELEZAJI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2007/2008

8. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa malengo kama yalivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya mwaka 2007/2008, umekuwa ukizingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar, ILANI ya Uchaguzi ya mwaka 2005 na Mpango wa matumizi wa muda wa kati (*Medium Term Expenditure Framework – MTEF)*.

9. **Mheshimiwa Spika,** wizara katika mwaka huo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 4,196,195,303.00 ambapo hadi mwezi Machi 2008 fedha zilizopatikana ni shilingi 2,808,313,689.00 sawa na asilimia 67. Kati ya hizo, shilingi 1,521,984,445.00 ni kwa mishahara na maposho (sawa na asilimia 67) na shilingi 1,286,329,244.00 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 67.3 ya makadirio.(*angalia kiambatisho namba1*). Kwa upande wa kazi za maendeleo, fedha zilizoidhinishwa ni shilingi 383,000,000 na hadi kufikia Machi 2008 fedha zilizopatikana ni shilingi 343,000,000.00 sawa na asilimia 89.56 ya makadirio. Kwa upande wa washirika wa maendeleo fedha zilizokadiriwa ni shilingi 1,531,649,000.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2008 ni shilingi 560,611,756.00 sawa na asilimia 36.6 ya makadirio. Kwa upande wa makusanyo ya mapato, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 201,970,000 ambapo hadi kufikia Machi 2007, shilingi 185,093,850 zilikusanywa sawa na asilimia 92 ya makadirio. *(angalia kiambatisho namba 3 na 4)*.

MALENGO YA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia 2007/2008, wizara kupitia taasisi zake mbalimbali imeweza kutekeleza

sehemu ya malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kama ifuatavyo:

I. Kuimarisha uwezo wa utendaji wa taasisi kwa kununua magari na pikipiki .
II. Kurahisisha upatikanaji wa Sheria kwa Kuchapisha na kusambaza Vitabu (volume) 12 na kutoa nakala 50 kila moja ya Sheria za Zanzibar kati ya mwaka 1980 hadi 2006.
III. Kuendesha mafunzo kwa wanasheria wa Serikali na waendesha Mashtaka.
IV. Kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zikiwemo za kuanzishwa Mahakama za watoto.
V. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa kukamilisha ujenzi wa Jengo la Afisi ya Mufti, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la maktaba ya makosa ya jinai na kufanyia matengenezo majengo na ofisi mbali mbali za Wizara na taasisi zake.
VI. Kutoa mafunzo na kutayarisha Muongozo wa Haki za Binaadamu kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar na
VII. Kuimarisha mfumo wa mashtaka kwa kuweka utaratibu wa kukamilisha upelelezi kabla ya kufungua kesi

MAFUNZO KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA

11. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara kupitia idara na taasisi zake imewasomesha jumla ya wafanyakazi wake 197. Kati ya hao, wafanyakazi 61 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 136 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi katika ngazi mbali mbali (*angalia kiambatisho namba 6a na 6b).*

UTEKELEZAJI MALENGO YA IDARA NA TAASISI

12. **Mheshimiwa Spika,** maelezo zaidi ya utekelezaji wa malengo kupitia Idara na Taasisi za Wizara kwa mwaka 2007/2008 ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO NA SERA

13. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii ndio yenye jukumu kubwa la kuratibu shughuli za Wizara. Jumla ya shilingi 479,657,000.00 ziliidhinishwa kwa mwaka 2007/2008 ambapo hadi kufikia Machi 2008 zilizopatikana ni shilingi 376,627,606 sawa na asilimia 79. Kati ya hizo shilingi 147,348,586 ni kwa mishahara na maposho sawa na asilimia 39 na shilingi 229,279,020 sawa na asilimia 61 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, kiasi cha shilingi 100,000,000.00 ziliidhinishwa ambapo fedha zote hizo zimepatikana. Kutokana na upatikanaji huo wa fedha, pamoja na kazi za kawaida Idara hii imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kuimarisha uwezo wa Idara katika kuratibu shughuli na kazi za Wizara

14. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza lengo hili Idara imenunua gari mbili ili kupunguza tatizo la usafiri pamoja na kununua vifaa vya kutendea kazi vikiwemo compyuta na samani. Kwa upande wa mafunzo Idara imewapeleka wafanyakazi wake 15 mafunzoni (wanawake 11 na wanaume 4). (Angalia kiambatisho 6a na 6b)

15. **Mheshimiwa Spika,** katika kutimiza majukumu yake ya kuratibu shughuli za Wizara, idara imeratibu mikutano mbalimbali ikiwemo ile ya Kamati ya Uongozi. Aidha mikutano ya watendaji wa taasisi juu ya utayarishaji wa maombi ya miradi, mipango ya mwaka, na ile ya kutayarisha

mipango ya Kimkakati kwa taasisi za wizara nayo iliratibiwa. Katika kuendeleza mashirikiano baina ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, SMZ, na Wizara ya Nchi (AR) Utawala Bora, SMT, mkutano mmoja ulifanyika huko Dar es Salaam mwishoni mwaka 2007.

16. **Mheshimiwa Spika,** idara pia imeendelea kuratibu utayarishaji wa taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya 2005, kwa kipindi cha miaka 2 kutoka Novemba, 2005 hadi Oktoba, 2007 na Utayarishaji wa taarifa za utekelezaji wa Miradi kwa kila mwezi (Julai hadi Disemba, 2007).

Kutekeleza malengo ya kupambana na UKIMWI

17. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea na mapambano dhidi ya ukimwi wizara iliandaa mafunzo ya wakufunzi wa taasisi zake Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwajengea uwezo wa kuendeleza mapambano katika taasisi zao. Hivyo basi taasisi zote sasa zinao wakufunzi wake wa kuwafundisha wafanyakazi mambo mbalimbali yahusuyo ukimwi. Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo wakufunzi hao kwa kila itapohitajika. Aidha kwa kushirikiana na Sauti ya Tanzania Zanzibar, Idara ilitayarisha na kurusha hewani vipindi vitatu vya kuelimisha umma juu ya haki za kisheria, kijamii na kiafya za watu wanaoishi na virusi vya ukimwi.

Kuendelea na kazi ya kulifanyia matengenezo jengo la Wizara

18. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchakavu wa muda mrefu wa jengo la Wizara, kazi hii ni ya kuendelea hatua kwa hatua kwa kadiri hali inavyoruhusu. Mbali ya kuhifadhi uimara wa jengo lakini pia tahadhari inachukuliwa kuhifadhi haiba ya kihistoria inayostahiki katika jengo hili.

Kuanzisha kitengo cha habari na kuanzisha tovuti ya Wizara

19. **Mheshimiwa Spika,** hatua za kuanzisha kitengo cha habari cha Wizara zimeanza ambapo kazi ya kutengeneza tovuti ya Wizara inaendelea. Kazi hiyo na inatarajiwa kukamilika sambamba na kumalizika kwa mwaka huu wa fedha. Kukamilika kwa tovuti hiyo kutawezesha wananchi na watu wengine ndani na nje ya nchi kupata habari mbalimbali zihusuzo utawala bora hapa Zanzibar. Aidha wananchi watapata fursa ya kutowa maoni yao au kuuliza masuala ya husuyo utawala bora na kupatiwa majibu yake.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Idara ya Mipango na Sera inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

I. Kuimarisha uwezo wa Idara katika kuratibu shughuli na kazi za Wizara;
II. Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI;
III. Kuendelea na kazi ya kulifanyia matengenezo jengo la Wizara; na
IV. Kutekeleza na kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kimkakati wa Wizara.

21. **Mheshimiwa Spika,** ili Idara ya Mipango na Sera iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 690,749,000.00 kwa kazi za kawaida

IDARA YA URATIBU UTAWALA BORA

22. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 100,407,000. 00 Kati ya

fedha hizo shilingi 26,308,000.00 ni kwa mishahara na maposho na shilingi 74,099,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi, 2008 fedha zilizopatikana ni shilingi 70,785,626.00 kati ya hizo shilingi 21,547,766.00 sawa na asilimia 82 ni kwa mishahara na maposho na shilingi 49,237,850.00 sawa na asilimia 66 kwa matumizi mengineyo.

23. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na upatikanaji huo wa fedha katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi 2008, Idara hii imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kukuza ushirikishwaji wa Taasisi za Kijamii katika shughuli za maendeleo.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika kuziimarisha taasisi za kijamii zoezi la kulipitia upya Daftari la Jumuiya Zisizo za Kiserikali limekamilika na tayari daftari hilo limeshazinduliwa. Kwa upande wa Sera ya Jumuiya, Sera hiyo ilijadiliwa upya kwa kuingizwa mapendekezo ya wadau mbalimbali. Ninafuraha kulijulisha Baraza lako kuwa hatua za kuipeleka Sera kwenye Baraza la Mapinduzi zimekamilika kupitia sekretatieti ya baraza. Aidha Idara katika kipindi cha miezi tisa imeweza kutayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi (36) vya redio vinavyoelimisha jamii katika shughuli za haki za binaadamu, utawala bora nk.

25. **Mheshimiwa Spika**, idara imeweza kushiriki katika mchakato wa kutafuta Jumuiya Bora ya Kiraia kwa maana yenye ufanisi mzuri Kitaifa na Kikanda. Zoezi hili lilifadhiliwa na Jumuiya ya " *Foundation For Civil Society*" mbali ya kutoa zawadi kwa Jumuiya bora Kitaifa na Kikanda zoezi hili linalenga katika kutoa ufahamu mkubwa zaidi juu ya majukumu ya Jumuiya

zisizo za Kiserikali na mchango wa jumuiya hizo katika harakati za kuleta maendeleo.

Kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Utawala Bora Zanzibar.

26. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza lengo hili idara imetayarisha na kujadili rasimu ya mfumo wa kutathmini shughuli za Utawala Bora katika Taasisi za Umma. Mikutano mitatu (3) ya washiriki wakuu wa Utawala Bora imefanyika. Idara pia kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) imeweza kuanza matayarisho ya uundwaji wa Kamati za Utawala Bora Kisekta, hatua ambayo imeanza kwa kutoa mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini juu ya viashiria vya Utawala Bora (Monitoring and Evaluation) kwa taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali.

27. Mheshimiwa Spika, idara katika mwaka wa fedha 2007/2008 imeanza kazi ya kuratibu upya mapitio ya Rasimu ya Sheria ya Kupambana na Rushwa. Aidha imeanza kazi ya kuratibu utayarishaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa na Maadili ya Viongozi. Hatua za awali za utekelezaji wa kazi hii zimeanza kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa.

28. Mheshimiwa Spika, katika kujenga uwezo wa watendaji kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Utawala Bora, idara imeendelea kuwaendeleza wafanyakazi wake kitaaluma kwa kuwapeleka masomoni wafanyakazi wake wawili wanawake katika mafunzo ya muda mrefu ya Stashahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii. Aidha wafanyakazi watatu walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Kukuza uelewa wa Wananchi juu ya masuala ya haki za Binaadamu

29. **Mheshimiwa Spika,** muongozo wa Haki za Binaadamu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 umetayarishwa kwa msaada wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Kazi ya utayarishaji iliwashirikisha wahusika mbali mbali wa Haki za Binaadamu na Utawala Bora, zikiwemo Jumuiya Zisizo za Kiserikali. Aidha kazi ya kuchapisha muongozo huo imekamilika na jumla ya vitabu 1600 vimechapishwa. Idara imelenga kwa sasa kuwafikia wananchi mijini na vijijini kutoa elimu ya Haki za Binaadam, na kuwasilishwa kwao Muongozo huo.

30. **Mheshimiwa Spika,** idara pia imetayarisha vipeperushi kwa ajili ya utoaji wa elimu ya Utawala Bora likiwemo suala la Haki za Binaadamu. Vipeperushi hivyo vitatolewa kwa wingi na kusambazwa katika jamii yetu ikiwa ni sehemu ya jitihada za Wizara na Serikali za kuwafahamisha wananchi haki na fursa zao za kikatiba.

31. **Mheshimiwa Spika,** idara imejipangia malengo yafuatayo kwa mwaka 2008/2009

    I. Kupanua uwelewa na utekelezaji wa Utawala Bora katika taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali.
    II. Kuendelea na kazi ya Uratibu wa Utawala Bora Zanzibar.
    III. Kuiimarisha idara ya Kuratibu Utawala Bora kitaaluma na Vitendea kazi.

32. **Mheshimiwa Spika,** ili Idara ya Uratibu Utawala Bora iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya

shilingi 117,790,000.00 kwa kazi za kawaida na shilingi 75,000,000.00 kwa kazi za maendeleo

MAHAKAMA

33. **Mheshimiwa Spika**, Mahakama Zanzibar katika bajeti ya 2007/2008 iliidhinishiwa jumla ya Shs. 1,169,700,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo Shs 755,420,000.00 ni kwa mishahara na maposho na Shs 414,280,000.00 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2008 fedha zilizopatikana ni Shs 729,058,826.00 kati ya hizo Shs 475,680,082.00 ni kwa mishahara na maposho sawa na asilimia 63% na Shs 253,378,744.00 sawa na asilimia 61% kwa matumizi mengineyo. Kwa kazi za maendeleo Shs. 10,000,000.00 zimepatikana kati ya Shs. 50,000,000.00 zilizokadiriwa. Kwa upande wa wahisani fedha zilizopatikana ni 21,875,750.00 sawa na asilimia 77.5 kati ya shilingi 28,222,650.00 zilizokadiriwa. Aidha Mahakama ilikadiria pia kukusanya Shs. 39,000,000.00 ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2008 fedha zilizokusanywa ni Shs. 27,885,852.00 sawa na asilimia 71.50% . *(angalia kiambatisho namba* 1 na 3).

34. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na upatikanaji huo wa fedha mahakama imeweza kutekeleza ahadi ilizozitoa kwa mwaka 2007/2008 na malengo yake ya mwaka 2007/2008.

Kwa upande wa utekelezaji wa ahadi, Mahakama iliahidi na kutekeleza mambo yafuatayo:

Udogo wa majengo la Mahakama za Mfenesini na Mwera

Kazi ya utanuzi wa jengo hili ilianza mwaka 2003/2004 kwa kutaka kuongeza ofisi mbili za Mahakimu, ghala, chumba cha washitakiwa nk. Kazi ambayo baadae ilisita kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo bado juhudi za kupata fedha

za kuendeleza kazi hiyo zinaendelea. Aidha hatua za ujenzi wa jengo la Mahakama hapo Mwera zinaendelea na hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kumpata mkandarasi baada ya kutangazwa kwa zabuni.

Kwa upande wa Mahakama ya kisasa eneo la Mkokotoni, ni kuwa eneo lililopo sasa ni finyu sana kwa shughuli za kimahakama, hata hivyo juhudi zinaendelea kupata eneo jengine katika Mkoa huo wa Kaskazini.

Tatizo la ucheleweshaji wa kesi

Kuchelewa kutoa maamuzi ya kesi kwa haraka hakusababishwi na Mahakama pekee, bali vyombo vyengine na wahusika tafauti pia wanahusika katika utaratibu mzima wa uendeshaji wa kesi vikiwemo Jeshi la Polisi, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, mawakili, mashahidi nk. Hata hivyo tatizo hili linatatuliwa kwa mashirikiano ya pamoja ya wahusika na vyombo nilivyovitaja. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuanzishwa vikao vya kamati ya kusukuma kesi 'caseflow management committees'.

Sambamba na Ahadi hizo Mahakama pia ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Mahakama Kuu Vuga na matengenezo madogo madogo kwa Mahakama Unguja na Pemba

35. **Mheshimiwa Spika,** ukarabati wa jengo la Mahakama Kuu Vuga umechukua muda mrefu tangu wafadhili wakubali kulifanyia matengenezo. Uchelewaji huo unatokana na taratibu za upatikanaji na matumizi ya fedha hizo za

wafadhili. Hatua iliofikiwa sasa ni kumpata msimamizi wa ujenzi ambae atasimamia ujenzi huo baada ya mkandarasi kuchaguliwa.

36. **Mheshimiwa Spika**, Mahakama kwa muda mrefu imekuwa inamiliki eneo hapo Mwanakwerekwe ambalo limetengwa mahsusi kwa ajili ya kujenga Afisi ya Mahakama ya Kadhi likiwa ni fidia kutokana na Mahakama iliyokuwepo hapo Rahaleo. Ili kulizuwia eneo hilo na kuondoa uwezekano wa kuvamiwa, Mahakama imejenga uzio kwenye eneo hilo. Aidha ramani na michoro ya kujenga jengo la Mahakama ya Kadhi imeshatayarishwa. Hatua za kutafuta wafadhili watakaosaidia ujenzi huo inaendelea.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika azma yake ya kuwa na majengo mapya na ya kisasa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, imeikabidhi Mahakama eneo pamoja na hatimiliki kwa ujenzi wa mahakama mpya huko Makunduchi. Viwanja vyengine vimepatikana maeneo ya Tunguu na Dunga. Hatua za kupatiwa hatimilki zinaendelea. Lengo ni kuwa na maeneo mapya ambayo yatatosha kujenga Mahakama za kisasa nchini.

Kuanza ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Mwera

38. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kazi za maendeleo, ujenzi wa Mahakama ya Mwera umeshaanza na unatarajiwa kumalizika ndani ya mwaka mpya wa fedha 2008/2009.

Kufanya tathmini ya mpango wa wahalifu kutumikia jamii

39. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kutungwa kwa Kanuni zinazohusiana na wahalifu kutumikia jamii na kuanza

kutumika kwa majaribio, tathmini haikuweza kufanyika kutokana na kuchelewa kuanza kwa mpango huo kwa vile maandalizi yake yalikuwa hajakamilika. Hivi sasa mpango umeanza kwa Mikoa ya Mjini/ Magharibi na Kusini Pemba na hadi kumalizika mwezi Machi 2008 ni mhalifu mmoja tu ambae amehukumiwa kutumikia adhabu hiyo.

Kuimarisha utendaji wa Mahakama kwa kuzipatia nyenzo na kuwaongezea taaluma wafanyakazi

40. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utendaji wa Mahakama, Makadhi wawili wa Wilaya pamoja na Mahakimu sita , watatu wa Wilaya na watatu wa Mahakama za mwanzo waliajiriwa. Katika kupiga vita rushwa Mahakama imefanya vikao na mahakimu na wafanyakazi wote kwa lengo la kusisitiza mapambano ya rushwa. Aidha wafanyakazi 15 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za cheti, stashahada, shada ya kwanza na ya pili. (angalia kiambatisho namba 6a)

Kupitia upya mfumo wa usimamizi wa Mahakama za Watoto

41. **Mheshimiwa Spika,** Hatua za kupitia mfumo wa usimamizi wa Mahakama za watoto zilichukuliwa kwa kuajiri mtaalamu kutoka Chuo cha Utawala na Uongozi wa Mahakama Lushoto. Mtaalam huyo alipendekeza kuwa Sheria mpya ya Mahakama za watoto iandaliwe kutokana na sheria iliyoko kuwa ya zamani sana na kuwa haiendani na mikataba mbali mbali ya Kimataifa ya haki za watoto. Aidha rasimu ya sheria mpya iliandaliwa na ilijadiliwa na wadau kutoka taasisi mbali mbali. Rasimu hiyo imeshawasilishwa katika Kamati ya Uongozi na kujadiliwa. Hivi sasa Mahakama inayafanyia kazi

mapendekezo ya Kamati ya Uongozi yaliyotolewa na hatimae kuwasilishwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu.

Usikilizaji na utoaji wa maamuzi

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kazi zake za kawaida Mahakama imeendelea na usikilizaji wa kesi na kutoa maamuzi. Katika mwaka huu wa fedha jumla ya kesi 4679 zilifunguliwa ambapo kesi 1151 ni za madai na kesi 3286 ni za jinai. Aidha rufaa za madai 164 na rufaa za jinai 78 zilifunguliwa (Angalia kiambatisho namba 7 i,ii,iii).

43. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama katika mwaka 2008/2009 imejiwekea malengo yafuatayo:

I. Kuendelea kufanyia matengenezo jengo la Mahakama Kuu Vuga.
II. Kuendelea na kufanya tathmini ya mpango wa wahalifu kutumikia jamii.
III. Kuimarisha utendaji wa mahakama kwa kuanzisha kamati ya kusukuma kesi (Case flow Management Committee).
IV. Kujenga jengo jipya la Mahakama huko Tunguu Unguja na kukarabati majengo ya zamani.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2008/2009 Mahakama ili itekeleze vyema shughuli zake inaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs 1,134,402,000.00 kwa kazi za kawaida na Shs 83,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha Mahakama katika mwaka huu imekusudia kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali mapato ya Shs 41,200,000.00.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuwa mshauri mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo yote ya kisheria. Afisi vile vile iliendelea na utekelezaji wa kazi zake nyingine za kawaida pamoja na kukamilisha malengo yaliyowekwa.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa jumla ya Shillingi 534,274,000.00. Kati ya hizo, shillingi 264,093,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na shillingi 270,181,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2008 fedha iliyopatikana ni shillingi 309,007,897.00, kati ya hizo shillingi 132,186,742.00 ni kwa mishahara na maposho sawa na asilimia 50% na Shillingi 176,821,155.00 sawa na asilimia 65% ni kwa matumizi mengineyo. Aidha Afisi ilipata ufadhili kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) wa jumla ya Shillingi 72,000,000.00 kwa ajili ya uchapishaji wa vitabu vya Sheria za Zanzibar, ununuzi wa baadhi ya vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kugharamia mafunzo kwa Wanasheria wa Serikali.

47. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na upatikanaji huo wa fedha, Afisi imeweza kutekeleza vizuri malengo yake. Hadi kufikia Machi, 2008 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Kuimarisha Ufanisi wa Utendaji kazi kwa kuwawezesha wafanyakazi kitaaluma pamoja na mambo mengineyo.

48. Mheshimiwa Spika, Afisi imeweza kusomesha wafanyakazi wanne (4), mmoja mafunzo ya Shahada ya Pili ya Sheria (LL.M) Uingereza na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi ya Kompyuta hapa Zanzibar. Vile vile Afisi imefanya Semina mbalimbali kwa ajili ya Wanasheria wake ili kuwapa ujuzi zaidi katika mambo yanayohusu sheria za biashara na mikakati ya kupambana na Rushwa. Aidha Afisi imeweza kupunguza tatizo la usafiri pamoja na vitendea kazi.

Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Serikali na Taasisi zake na jamii kwa Jumla.

49. Mheshimiwa Spika, hili ndilo jukumu kuu la Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Serikali imeendelea kushauriwa kwa hekima na busara kwa kuzingatia masharti na maelekezo ya Katiba ya Zanzibar pamoja na Sheria nyingine mbali mbali. Sambamba na jukumu hilo, Afisi imeweza pia kusimamia Kesi 29 za Madai kwa niaba ya Serikali katika Mahkama mbali mbali zikiwemo 2 katika Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.

Kutayarisha Miswada ya Sheria na Kanuni mbali mbali za Sheria.

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Afisi ya Mwanasheria Mkuu hadi kufikia Machi, 2008 imeweza kutayarisha na baadae kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu jumla ya Miswada ya Sheria 13. (angalia kiambatisho namba 12)

Kuchapisha Sheria za Zanzibar kutoka 1980 hadi 2006.

51. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na msaada wa UNDP Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeweza kuzichapisha Sheria za Zanzibar za kutoka mwaka 1980 hadi 2006. Vitabu hivyo vya Sheria vimegawiwa katika Wizara zote za Serikali, vituo vyote vya Polisi pamoja na Mahkama zote hadi ngazi ya Wilaya. Aidha, baadhi ya Taasisi zikiwemo Vyuo Vikuu na Vyama vya Wanasheria wamepatiwa Sheria hizo bila ya malipo. Afisi vile vile imeweza kwa mara ya kwanza kuchapisha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kwa lugha ya Kiingereza. Mpango huu ni miongoni mwa mikakati ya uimarishaji wa Utawala Bora ambao unasisitiza Utawala wa Sheria.

Kufanyia Mapitio Sheria za Zanzibar na Kupendekeza Marekebisho.

52. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa lengo hili ulidhamiria kuzifanyia mapitio Sheria mbali mbali za Zanzibar na hasa zile zilizotajwa katika Ripoti ya Nyalali kuwa zimepitwa na wakati. Kazi hiyo inaendelea kufanywa na Sekretariati ya Tume ya Kuchunguza Sheria na matokeo ya mapitio yatawasilishwa Serikalini baada ya kukamilika.

Kuendelea Kuimarisha Tume ya Kuchunguza Sheria.

53. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa changamoto kubwa katika kuimarisha Tume ni ukosefu wa Afisi ya kufanyia kazi. Changamoto hii inaendelea kushughulikiwa, kwanza kwa ujenzi wa Jengo dogo la Afisi kama ni njia ya mpito na baadae kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Jengo rasmi la Afisi ya Tume. Hivi sasa Tume imepatiwa ofisi katika jengo la Wizara baada ya kuwahamisha baadhi ya watendaji wa

Idara ya Mipango na kuwapeleka katika jengo hilo dogo la Tume kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu ilivyoelekeza.

54. Mheshimiwa Spika, Tume katika mwaka wa 2007/2008 imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wanasheria wake wawili. Aidha, Tume imeweza kukamilisha utafiti kuhusu adhabu ya kifo na kuwasilisha mapendekezo yake katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Kazi za Tume zinatazamiwa kuimarika zaidi katika mwaka wa 2008/2009 kwa kuteuliwa Makamishna, kuongeza wafanyakazi pamoja na vifaa vya kazi.

55. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaazimia kutekeleza malengo yafuatayo:-

I. Kukamilisha kazi za uchapishaji wa Sheria za 2007 na 2008 pamoja na Sheria ndogo ndogo (Subsidiary Legislations) za 1980– 2008;
II. Kuendelea na uimarishaji wa Tume ya Kuchunguza Sheria pamoja na utendaji wa kazi zake.
III. Kuanza matayarisho ya ujenzi wa Jengo jipya la Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

56. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza kazi na malengo yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, naliomba Baraza lako tufuku kuidhinisha jumla ya Shilingi 550,450,000.00 Kwa kazi za kawaida na Shillingi 200,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

57. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2007/2008 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya shilingi 435,100,000.00 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 170,100,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho, na shilingi 265,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2008, fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara na maposho ni shilingi 132,992,236.00 sawa na asilimia 78 na kwa matumizi mengineyo ni shilingi 198,172,110.00 sawa na asilimia 74. Kwa shughuli za maendeleo fedha zilizoidhinishwa ni 200,000,000.00 ambazo zimepatikana zote.

58. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2007/2008, Afisi iliendelea na kazi zake za kawaida na kukamilisha malengo iliyowekewa. Mkazo mkubwa uliwekwa katika kuimarisha usimamizi wa mashtaka, uwezo wa watendaji, vifaa pamoja na mazingira ya kufanyia kazi. Kwa upande wa usimamizi wa mashtaka, hadi kufikia Machi, 2008 jumla ya kesi zote zilizofunguliwa katika Mahkama zinazosimamiwa na Ofisi hii Unguja na Pemba ni 830. (angalia kiambatisho namba 13)

59. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa usimamizi wa mashtaka huko Pemba hadi kufikia Machi 2008, Mahkama ya Mkoa ya Chake Chake imefungua kesi 42 na Mahakama ya Wete kesi 59.

60. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na ufunguaji na usimamizi wa kesi, afisi imeendelea kutoa ushauri kwa wapelelezi wa makosa ya jinai. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2008 jumla ya majalada 208 yamepokelewa kutoka Jeshi la Polisi na

kupatiwa ushauri. Kati ya hayo 204 ni kutoka Unguja na 4 yanatoka Pemba.

61. **Mheshimiwa Spika,** Mbali na utekelezaji wa kawaida, Afisi imechukuwa jitihada ya utekelezaji wa malengo yake ili kuleta ufanisi katika kazi. Hadi kufikia Machi, 2008 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Afisi

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake, Afisi imewapatia mafunzo watumishi 29 katika kada tofauti zikiwemo za sheria, utawala, utunzaji wa kumbukumbu, n.k katika ngazi za cheti, stashahada ya kawaida na shahada ya pili. (Angalia Kiambatisho 6a na 6b)

Kudumisha uhusiano bora kati ya wadau wa kesi za jinai

63. **Mheshimiwa Spika,** Afisi inaendelea kudumisha uhusiano miongoni mwa wadau wa kesi za jinai. Kwa kipindi cha July 2007 mpaka Machi 2008 vikao 6 vimefanyika vilivyojumuisha Wakuu wa Upelelezi Mikoa, Makao Makuu, Usalama Barabarani, Madawa ya Kulevya na Kitengo cha Wizi wa Mali za Serikali. Mbali na vikao hivyo, maafisa wa Afisi hii wamefanya ziara za kikazi katika maeneo tofauti na kupata fursa ya kujadiliana na wadau mbali mbali kwa kuleta ufanisi wa kazi ya uendeshaji wa Mashtaka ya jinai.

64. **Mheshimiwa Spika,** Afisi iliandaa Mkutano 1 wa mwaka, ambao ulifanyika Disemba 2007. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kufanya tathmini ya uendeshaji mashtaka. Mkutano huo pia ulijumuisha wadau wa masuala ya kesi za jinai.

Miongoni mwa wadau hao ni Polisi, Mahakama, Mawakili wa kujitegemea, Chuo Cha Mafunzo, Ofisi ya Mkemia Mkuu n.k.

Kuimarisha huduma za Maktaba

65. **Mheshimiwa Spika,** Afisi hii inaendelea na uimarishaji wa huduma za Maktaba ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi 2008, imepokea vitabu vyenye thamani ya fedha za Kitanzania shilingi milioni 28,600,000 ambavyo vimenunuliwa kwa msaada wa UNDP. Vitabu hivyo ni kwa ajili ya kuimarisha maktaba ndogo ya Pemba na pia maktaba ya Ofisi kuu. Aidha msimamizi wa maktaba pia amemaliza mafunzo ya Stashahada ya kawaida ya Sheria (Diploma) kutoka Chuo Cha Uongozi wa Mahakama kilichopo Lushoto - Tanga .

Kukamilisha utanuzi wa majengo ya Afisi

66. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu ya Afisi kufikia uendeshaji wa mashtaka katika Wilaya, Afisi imefanya kazi ya kutanua na kutafuta maeneo kwa ajili ya uendeshaji wa kesi katika Mahkama tofauti za Mikoa na za Wilaya. Hadi kufikia Machi 2008, afisi imekamilisha ujenzi sehemu ya chini (ground floor) wa jengo lililopo pembezoni mwa jengo la Afisi ya sasa ambalo litatumika kwa kutolea huduma ya Maktaba na Afisi. Aidha, Afisi imefanya ukarabati wa jengo liliopo Mwanakwerekwe ambalo litatumika kuwa Afisi za waendesha mashtaka wa Wilaya. Jengo hilo limekamilika kwa hatua za mwanzo. Afisi imeweza pia kufanya ukarabati wa chumba cha mashtaka ndani ya jengo la Mahakama ya Wete. Aidha Afisi imeweza kupata jengo kutoka ZSTC na kulikarabati ambalo sasa linatumiwa na waendesha mashtaka katika Mahakama za Mkoani Pemba.

Kuimarisha mfumo wa uendeshaji Mashtaka kwa kujenga utaratibu wa kukamilishwa upelelezi kabla ya kufungua mashtaka

67. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeanza hatua ya kukamilisha lengo la kuimarisha mfumo huo ambapo, hadi kufikia Machi 2008 Afisi imekutana na wahusika wa upelelezi na kuona namna ya kuikamilisha azma hii. Kwa baadhi ya kesi, utaratibu huu umeanza kutumika. Utaratibu huu umeanza kuonyesha dalili za wazi za kupunguza mlundikano wa kesi, wingi wa mahabusu na kupunguza ucheleweshaji wa kesi. Tathmini rasmi itafanywa mwishoni mwa mwaka huu ili kuona mafanikio na matatizo yake.

Kukamilisha hatua ya pili ya mpango wa uendeshaji wa mashtaka katika ngazi ya Wilaya (Roll out of Civilianization to Districts)

68. **Mheshimiwa Spika,** katika kukamilisha hatua ya pili ya uendeshaji Mashtaka ngazi za wilaya, hadi kufikia Machi 2008, Afisi imefanya matayarisho kwa kuwa na Afisi ambazo zitatumiwa na waendesha mashtaka kwa Mahakama za Wilaya za Mwanakwerekwe, Wete na Mkoani. Aidha wanasheria 7 wameajiriwa, watano kati yao wapo Unguja na 2 wapo Pemba. Katika kuhakikisha upatikanaji mzuri wa mashirikiano ambao utaimarisha uendeshaji wa mashtaka ya jinai, Afisi imefanya mikutano kadhaa iliyoshirikisha waendesha mashtaka wa Mahkama za Wilaya na Jeshi la Polisi.

Uanzishwaji wa tovuti (Website) ya Afisi

69. **Mheshimiwa Spika,** hatua iliyofikiwa katika kutekeleza lengo hili hadi mwezi wa Machi, 2008 ni kuteua kampuni ya kufanya kazi hiyo na kutayarisha taarifa mbali mbali ambazo zitaingizwa katika tovuti hiyo na kuweza kuwa njia ya kubadilishana taarifa na taasisi za nje pia.

70. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Afisi hii na mfumo mzima wa utoaji haki za jinai bado unakabiliwa na changamoto nyingi na kubwa. Miongoni mwa changamoto hizo ni, kuchelewa kesi, kupungua kwa uadilifu, utaalamu na vifaa duni katika ngazi zote za utoaji haki. Malengo ambayo Afisi imejiwekea kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ni sehemu ya juhudi ya kukabiliana na changamoto hizo.

Kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria za Jinai na Sheria ya Ushahidi.

71. **Mheshimiwa Spika**, Afisi imekamilisha matayarisho ya awali kwa kupata fedha katika mradi wa "Strengtherning Transparency Intergrity and the rule of law" chini ya udhamini wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa UNDP. Mapitio ya Sheria za Jinai na Sheria ya Ushahidi yanatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwaka ujao wa fedha.

72. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeazimia kutekeleza malengo yafuatayo:-

    I. Kuimarisha uwezo wa utendaji wa ofisi

II. Kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa mashtaka kwa kujenga utaratibu wa kukamilishwa upelelezi kabla ya kufungua mashtaka,

III. Kuandaa mapendekezo ya mpango wa pamoja wa usimamizi wa jinai (Zanzibar Criminal Justice Framework),

IV. Kufanya tathmini ya usimamizi wa Mashtaka na kutoa taarifa ya mwaka 2008,

V. Kukamilisha na kuimarisha hatua ya tatu ya mpango wa uendeshaji mashtaka katika ngazi ya wilaya (Roll out civilization), na

VI. Kuandaa mapendekezo ya mapitio ya Sheria za jinai, sheria ya ushahidi na sheria ya Afisi ya uendeshaji wa mashtaka.

73. Mheshimiwa Spika, Ili kuiwezesha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itekeleze majukumu yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, ninaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 508,000,000.00 kwa kazi za kawaida na shilingi 300,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU

74. Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Afisi hii ni kuzifanyia ukaguzi fedha zote zinazotolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kutoa taarifa zake za ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Afisi imekamilisha ripoti ya ukaguzi wa hesabu ya mwaka 2006/2007 na ripoti hiyo tayari imewasilishwa katika Baraza lako tukufu, ili ipate kufanyiwa kazi na Kamati ya kuchunguza Hesabu za Serikali (PAC). Aidha ukaguzi wa hesabu za mwaka 2007/2008 unaendelea na ni matumaini yetu kwamba utakamilika kwa wakati na kutoa ripoti kwa mujibu wa sheria.

75. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kazi za ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo kwa mwaka 2007/2008, Afisi imeweza kupiga hatua kubwa ya kuondoa mrundikano wa mafaili ya wastaafu. Hali hii imepelekea wastaafu kuweza kulipwa mafao yao ya viinua mgongo na pencheni kwa wakati. Aidha Afisi inaendelea kutoa muongozo na elimu kwa maafisa watendaji wanaotayarisha mafao ya wastaafu, fidia n.k ili kuondoa dosari mbali mbali zinazobainika wakati wa ukaguzi wa mafaili hayo. Kutokana na juhudi hizi Serikali imeweza, kupunguza madeni ya viinua mgongo na pencheni kwa wastaafu kwa asilimia kubwa katika kipindi hiki.

76. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka wa fedha 2007/2008 iliidhinishiwa jumla ya Shs 667,300,000.00 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Shs 460,316,000.00 ni kwa mishahara na maposho na Shs 206,984,000.00 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2008 fedha zilizopatikana ni Shs 409,458,091.00 sawa na asilimia 61, kati ya hizo Shs 253,806,441.00 ni kwa mishahara na maposho sawa na asilimia 55, na Shs 155,651,650.00 sawa na asilimia 75 kwa matumizi mengineyo (angalia kiambatisho namba 1). Kwa upande wa kazi za maendeleo Shs. 33,000,000.00 ziliidhinishwa ambapo fedha zote hizo zimepatikana. (angalia kiambatisho namba 5).

77. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na upatikanaji huo wa fedha, pamoja na kazi za kawaida Afisi hii imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kufanya ukaguzi katika taasisi zote za Serikali na kutoa taarifa za ukaguzi huo kwa wakati.

78. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Afisi imeweza kuendelea kufanya ukaguzi katika taasisi zote za Serikali pamoja na Halmashauri za Wilaya na tunategemea kuwa taarifa za ukaguzi huo zitatoka kwa wakati uliopangwa na kwa mujibu wa sheria. Afisi pia imeweza kutoa ushauri wa kitaaluma kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya juu ya uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali kwa kufuata sheria za hesabu, hali ambayo imeleta mafanikio mazuri na kumekuwa na tofauti kubwa ya hoja zilizotolewa kwa kulinganisha na kipindi kilichopita. Pia Afisi imefanikiwa kuwapatia wafanyakazi wake 106 mafunzo mbali mbali ya muda mfupi na mrefu. (angalia kiambatisho 6a na 6b)

Kuendeza uhusiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali ya Muungano Tanzania.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2007/2008, Afisi kwa kushirikiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Muungano imefanya ukaguzi wa pamoja katika taasisi mbali mbali kama vile, mradi wa MACEMP, PADEP, mradi wa UKIMWI na miradi mingine inayofadhiliwa na washirikai wa Maendeleo. Afisi pia imefanya ziara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali ya Muungano na ujumbe wake kuja Zanzibar ili kuhamasisha ushirikiano uliopo. Aidha Afisi imewapeleka wafanyakazi kumi (10) kushiriki mafunzo kwa vitendo katika fani mbali mbali.

Kujiunga na Jumuia za kimataifa za INTOSAI na AFROSAI-E.

80. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haikufanikiwa kupata uanachama wa moja kwa moja katika jumuiya hizo kutokana na sababu

kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tayari ni mwanachama wa jumuiya hizo. Pamoja na hayo Afisi inapata faida na huduma mbalimbali zinazotolewa na jumuiya hizo ikiwemo mafunzo, kushiriki katika semina, mikutano na makongamano, na kupatiwa majarida mbalimbali.

81. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji mapato; Afisi ilikadiriwa kukusanya Shs.4,000,000.00 na hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2008 fedha zilizokusanywa ni Shs 2,700,000.00 sawa na asilimia 67.5 ya makadirio. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Afisi imekusudia kukusanya na kuchangia katika mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya Shs 4,000,000.00.

82. Mheshimiwa Spika: Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

I. Kufanya ukaguzi katika taasisi za Serikali pamoja na miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na kuhakikisha taarifa za ukaguzi zinatoka kwa wakati,

II. Kuendeleza mashirikiano baina ya Afisi yetu na Afisi nyengine za ukaguzi duniani pamoja na mashirika ya maendeleo,

III. Kujenga uwezo wa Afisi kiutendaji, kimazingira na kielimu; na

IV. Kujenga uwezo na uhusiano mzuri na wadau wetu mbali mbali, ikiwemo PAC na Taasisi nyenginezo.

83. Mheshimiwa Spika: ili afisi iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2008/2009 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shillingi 900,000,000.00

kwa kazi za Kawaida na Shillingi 120,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR

84. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2007/2008, Afisi ya Mufti wa Zanzibar iliidhinishiwa jumla ya shilingi 98,601,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 63,884,000.00 ni kwa mishahara na maposho na shilingi 34,717,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2008, fedha zilizopatikana ni shilingi 79,372,322.00. Kati ya hizo, shilingi 53,489,827.00 ni kwa mishahara na maposho ambazo ni sawa na asilimia 84%, na shilingi 25,882,495.00 sawa na asilimia 75% kwa matumizi mengineyo (Angalia kiambatanisho Nam 1)

85. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kazi za maendeleo kiasi cha shilingi 25,000,000.00 ziliidhinishwa ambapo hadi kufikia mwezi Machi fedha zote hizo zimepatikana na kuchangia katika kazi ya ujenzi wa ukuta wa kuzunguuka jengo jipya la ofisi. Aidha ofisi ilikadiria kupata shillingi 230,000,000.00 kwa ujenzi wa ofisi kutoka Serikali ya Oman ambazo nazo zimepatikana zote. Katika kipindi hicho Afisi pia ilikadiria kupata msaada wa shilingi 84,500,000.00 kutoka Benki ya Dunia na 'Global fund' kupitia ZAC kwa ajili ya kampeni dhidi ya Ukimwi. Kati ya fedha hizo zilizopatikana ni shilingi 71,888,000.00 sawa na asilimia 85.1%.

Afisi hii imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kukamilisha jengo la Afisi ya Mufti wa Zanzibar

86. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo hili tayari umekamilika pamoja na kwamba kazi ilichukua muda mrefu kuliko ilivyopangwa. Hali hii ilikuwa nje ya uwezo wa Wizara. Hivi sasa mawasiliano yanaendelea baina ya Afisi ya Mufti wa Zanzibar na Afisi ya Mufti wa Oman kupitia kwa Ubalozi mdogo wa Oman uliopo Zanzibar, kupanga juu ya makabidhiano ya jengo hilo na pia ufunguzi wake rasmi.

Kuendelea kutoa Fatwa na kujibu masuala ya waislam

87. **Mheshimiwa Spika**, Afisi hii imepokea hoja na maswali mengi kutoka kwa wananchi ndani na nje ya Zanzibar. Hadi Machi, 2008 jumla ya maswali 415 yalipokelewa kutoka Tanzania Bara na maswali 247 yalipokelewa kutoka Zanzibar. Kati ya maswali hayo kutoka Bara na Zanzibar, yaliyojibiwa ni 483 na yaliyosalia bado yanafanyiwa kazi. Kwa upande wa migogoro ya kidini, jumla ya migogoro 367 ilipokelewa kutoka maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati ambapo migogoro 306 imepatiwa ufumbuzi, migogoro 7 ilibidi ipelekwe Mahakama za Kadhi za Wilaya. Migogoro 5 imerejeshwa Makao Makuu ya BAKWATA kwa vile ilitokea Tanzania Bara, na 7 imepelekwa Wizara ya Wanawake na watoto na iliyosalia bado ipo mezani kwa kupatiwa ufumbuzi.

Kuendelea kushirikiana na Mashirika mbali mbali ya kidini ndani na nje ya nchi

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008, Afisi imezidi kuheshimika na kutambulika hadi nje ya Nchi kutokana na juhudi zake za kuhimiza na kusimamia Amani na

Utulivu Nchini. Kamati za dini tofauti zinazoshughulikia Amani na Utulivu na ile ya UkIMWI zimezidi kuimarika, na sasa kuna kamati ndogo ndogo hadi katika Shehia. Tayari mikutano mbali mbali ya Kamati ya Amani imeshafanyika hapa Unguja na hivi sasa maandalizi yanaendelea kwa kamati hiyo kukutana na Shehia za Pemba. Baadhi ya Taasisi toka nje ya Nchi zilizotembelea Afisi ya Mufti wa Zanzibar hadi Machi, 2008 ni pamoja na Kikundi cha Wamishonari kutoka Canada, Kikundi cha wachungaji kutoka Denmark, Taasisi ya wanaharakati wa UKIMWI cha TALAWADOG kutoka Hargeisa – Somaliland, Taasisi ya Sebil Foundation kutoka Uturuki, na pia Ujumbe wa Kidini (Waislamu na Wakristo kutoka Uingereza).

Kuendelea na Mapambano dhidi ya Ukimwi kwa taratibu za kiislam.

89. **Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Mufti wa Zanzibar katika mwaka huu wa fedha imeendelea kuwafunza wanawake wa Kiislamu juu ya kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI majumbani (Home based care). Pia afisi imeweza kuanzisha Kamati za UKIMWI katika Wilaya 4, mbili Unguja na mbili Pemba. Aidha afisi imeweza kupata gari kwa msaada wa Benki ya Dunia (World Bank), kupitia Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC). Kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la BALM IN GILEAD, Afisi imeweza kuendeleza mafunzo kwa Walimu wa Madrasa juu ya matumizi ya mtaala wa UKIMWI. Aidha afisi imegawa vipeperushi vyenye ujumbe wa kujikinga dhidi ya UKIMWI na kuvigawa kwa wadau mbali mbali.

90. **Mheshimiwa Spika**, Afisi kwa kushirikiana na shirika hilo la Balm in Gilead, imeweza kuwatambua watoto mayatima na

wanaoishi katika mazingira magumu na kuwasaidia kifedha, sare za skuli, kuwapa vyakula na vifaa vya kuandikia. Kwa kuanzia, mradi huu umeanza kutekelezwa katika Wilaya za Kaskazini "A" Unguja na Micheweni kwa Pemba.

Kufanya utafiti wa kitaalamu kutafuta vyanzo vya migogoro ya kidini Zanzibar.

91. Mheshimiwa Spika, timu ya Wataalamu iliyoteuliwa imekamilisha kazi ya utafiti huo na kukabidhi ripoti yake mwishoni mwa mwaka jana. Utafiti huo umeweza kutoa sura halisi juu ya vyanzo hivyo na tayari Wizara yangu imepokea utafiti huo na inaufanyia kazi.

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 Afisi imejiwekea malengo yafuatayo:-

I. Kuimarisha elimu ya Dini katika Jamii ya Kiislamu ndani na nje ya nchi,
II. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi,
III. Kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa taratibu za Kiislamu.

93. Mheshimiwa Spika, ili afisi hii iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea kwa ufanisi zaidi kwa mwaka huu wa fedha wa 2008/2009, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 136,774,000.00 kwa kazi za kawaida na shilingi 25,000,000.00 kwa kazi maendeleo.

AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

94. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla

ya shillingi 185,916,000.00, ambapo mishahara na maposho ni 101,317,000.00 na shilingi 84,599,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2008 fedha zilizopatikana ni shilingi 150,681,900.00, ambapo shillingi 90,440,366.00 sawa na asilimia 89 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 60,241,534.00 sawa na asilimia 71 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa mapato, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inavyo vianzio vinane ambavyo kwa mwaka 2007/2008 ilikadiriwa kukusanya shilingi 158,970,000.00, kwa kipindi cha miezi tisa (Julai – Machi) afisi imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 154,507,998.00 ambayo ni sawa na asilimia 97 ya makadirio (kiambatisho namba 3 na 4*)*. Pamoja na utekelezaji wa kazi za kawaida, Afisi hii iliendelea kutekeleza kwanza ahadi iliyoitoa kwa mwaka 2006/2007 na malengo ya mwaka 2007/2008 kama ifuatavyo:-

95. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa ahadi, Afisi iliendelea kutekeleza ahadi ya mwaka 2006/2007 ya kuiimarisha afisi kwa kuipatia vitendea kazi vya kisasa.

Katika utekelezaji wa ahadi hii, Afisi imepata komputa nane (8) kupitia ufadhili wa Shirika la maendeleo la Umoja wa mataifa (UNDP). Aidha katika kipindi cha mwaka 2007, Afisi imepokea pikipiki mbili (2) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Afisi yenyewe kununua kompyuta mbili (2) na printer moja (1). Vifaa vyote hivi vimeshapelekwa kunakohusika zikiwemo kompyuta kwa kila Wilaya kwa kazi za usajili. Aidha, Afisi inatarajia kupokea seti mbili za computer, mashine moja ya kutolea photokopi na scanner ambavyo vinasubiri makabidhiano. Afisi inatarajia kupata vitendea kazi zaidi kupitia mradi wa kuimarisha mazingira ya biashara wa BEST.

Afisi ya Mrajis iliweza kutekeleza malengo ya mwaka 2007/2008 kama ifuatavyo:-

Kuzifanyia marekebisho Sheria mbali mbali

96. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Afisi imefanikiwa kuandaa sheria ya tasnia ya mali za ubunifu (Industrial Properties) ambayo tayari imeshajadiliwa na kupitishwa na Baraza lako tukufu. Sheria hiyo hivi sasa inasubiri saini ya Mheshimiwa Rais ili itumike rasmi. Sheria hiyo mpya inalenga katika kuimarisha mifumo ya usajili na ulinzi wa mali za ubunifu ikiwa ni pamoja na kuzingatia misingi na vigezo vya kimataifa vya ulinzi huo kwa maslahi ya Zanzibar.

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine Afisi tayari imeshandaa rasimu ya Sheria ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na hivi sasa rasimu ipo katika hatua ya kupata maoni ya wadau kabla ya kuipeleka katika vikao vya juu kwa hatua zaidi. Aidha kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania – MKUMBITA (BEST Program), Afisi inategemea kuandaa na kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zote zinazoongoza usajili na uendeshaji wa biashara ambapo kazi ya kuzirekebisha sheria za usajili wa makampuni, nyaraka na mali zinazohamishika itafanywa.

Kuimarisha utendaji katika ngazi ya Makao Makuu, Wilaya na Masheha;

98. **Mheshimiwa Spika,** Afisi kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji Zanzibar imeweka mikakati ya kutafuta mbinu za muda mfupi na mrefu za kupambana na udanganyifu katika utengenezaji wa vyeti vya kuzaliwa na pasi za kusafiria sambamba na

kuvitambua vyeti bandia vya kuzaliwa. Hata hivyo mafunzo maalum kwa makatibu wa masheha, ambayo yalikuwa yafanyike kwa ushirikiano na Shirka la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), hayakuweza kufanyika. Mafunzo hayo sasa yanatarajiwa kufanyika mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Kuwapatia mafunzo na kujenga uwezo wa watendaji

99. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 wafanyakazi watano (5) wamejiunga na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo tofauti vya ndani ya nchi kwa ngazi na fani tofauti ikiwemo sheria, utawala, uhasibu na takwimu. Idadi hiyo imefanya jumla ya wafanyakazi walioko masomoni kufikia kumi na mbili (12). Aidha, wafanyakazi wawili wamehudhuria mafunzo mafupi juu ya usimamizi wa miradi, mmoja alikwenda kwenye ziara ya mafunzo huko Nairobi, Kenya, mmoja amehudhuria mafunzo mafupi Japan yanayohusiana na Mali za Ubunifu (Intellectual Property Rights for Africa). Na mfanyakazi mmoja amehudhuria mafunzo mafupi huko Sweden.

Kuimarisha mifumo ya usajili wa nyaraka na uingizaji wa kumbukumbu za vizazi na vifo katika kompyuta.

100. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Afisi imeingiza kumbukumbu (data) za vizazi za mwaka 2006 za Wilaya ya Mjini na Magharibi na kazi ya uingizaji wa kumbukumbu za Wilaya ya Kusini kwa mwaka huo huo imeanza.

Kazi za Usajili.

101. Mheshimiwa Spika, jumla ya Vizazi 29,751 vimesajiliwa Unguja na Pemba, ambapo wanaume ni 15,299 na

wanawake ni 14,452, hadi kufikia Machi 2008, ambapo vyeti 20,075 vimetolewa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa kipindi hicho hicho. Aidha jumla ya vifo 1,939 vimesajiliwa ambapo wanaume ni 1,024 na wanawake ni 915. Kwa upande wa urithi kwa wasiokuwa waislamu, jumla ya "*estate duty*" 57 na Tirka 10 zilishughulikiwa. Aidha katika kipindi hicho pia yamesajiliwa Makampuni 192, Majina ya Biashara 288, jumuiya zisizo za kiserikali (NGOs) 72, alama za Biashara (*Trade Marks*) 404, na Alama za Uvumbuzi (Patents) 7.

102. Mheshimiwa Spika, Idadi ya nyaraka zilizosajiliwa katika kipindi cha Julai 2007 – Machi 2008 ni 1110 ambapo nyaraka 1016 zimesajiliwa Unguja na nyaraka 94 zimesajiliwa Pemba. Kwa upande wa ndoa na talaka, Jumla ya mabuku 105 ya ndoa yametolewa katika kipindi cha Julai 2007 – Machi 2008, wakati mabuku 9 ya talaka yametolewa katika kipindi hiki ambayo yametumika katika wilaya tofauti za Unguja.

103. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009.

I. Kuimarisha uwezo wa ofisi kiutendaji,
II. Kuendelea kuzifanyia marekebisho Sheria mbali mbali zinazosimamiwa na Afisi,
III. Kuimarisha utumiaji wa teknolojia katika mifumo ya usajili,
IV. Kutoa elimu ya shughuli za Afisi ya Mrajisi kwa wadau na wanachi kwa ujumla

104. Mheshimiwa Spika, ili Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa mwaka 2008/2009, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 270,580,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

AFISI YA MSAJILI HAKIMILIKI

105. Mheshimiwa Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ina majukumu ya kulinda na kusimamia haki na maslahi ya wasanii wa Zanzibar kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki (Nam. 14) ya mwaka 2003. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/ 2008 Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya shilingi 114,000,000.00 ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2008 shilingi 83,840,000.00 zimepatikana ikiwa ni sawa na asillimia 73.5. Kutokana na upatikanaji huo wa fedha, Afisi hii imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kuimarisha mfumo wa usajili na kuanza utoaji wa leseni.

106. Mheshimiwa Spika, katika kufikia lengo hili Afisi imeweza kuandaa kanuni za utoaji leseni. Wahusika wa leseni hizo ni watumiaji wote kibiashara wa kazi za sanaa wakiwemo vyombo vya habari, mahoteli, kumbi za starehe na burudani n.k. Kwa kuanzia leseni hizo zitatolewa kwa vyombo vyote vya habari vya Serikali na vya watu binafsi. Watumiaji hao wanategemewa kuanza kulipia matumizi hayo kuanzia mwezi Julai, 2008.

107. Mheshimiwa Spika, Jumla ya kazi arobaini na sita za sanaa zimesajiliwa zikiwemo za muziki, vitabu/miswada na mashairi. Kazi zote zimesajiliwa kwa kutumia mfumo maalum wa elektroniki. Kuongezeka kwa usajili wa kazi za sanaa kunatokana na kukuwa kwa kiwango cha uelewa kwa wasanii na wananchi kufuatia taaluma inayotolewa na Afisi.

Kuendelea kuelimisha jamii juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki

108. Mheshimiwa Spika, Afisi inaendelea na jukumu lake la kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari, warsha, semina na mazungumzo ya ana kwa ana. Afisi tayari imeshawafikia watendaji wa mikoa na wilaya zote za Zanzibar kueleza dhana hii ya Hakimiliki na Sheria husika. Vipindi tisa vya televisheni vilitayarishwa na kurushwa hewani.

109. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2008, warsha sita ziliendeshwa. Warsha hizo ziliwahusisha wasanii, watumiaji wa kazi za sanaa na uongozi wa Jeshi la Polisi Zanzibar. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ambao ni wahusika muhimu wa Hakimiliki, Afisi imeweza kuendesha warsha nne kwa watendaji mbali mbali wa Wizara hiyo wakiwemo, makamishna, wakurugenzi, wenyeviti wa mabaraza, maafisa wa utamaduni wa Wilaya na Mikoa, na watayarishaji wa vipindi pamoja na watangazaji.

Kuimarisha Afisi kiutendaji.

110. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza lengo hili, Afisi imeamua kuwa na mifumo miwili ya usajili na uhifadhi mzuri wa kazi za sanaa Zanzibar kwa Unguja na Pemba na kuanza kazi rasmi mwezi Juni mwaka huu. Hii ni kwa ajili ya urahisi na ufanisi na hasa kwa kuzingalitia hali na uwezo wa wasanii. Afisi imeweza kupanua shughuli zake Pemba baada ya kupatikana Afisi na wafanyakazi. Aidha maofisa wengine wawili wameajiriwa kwa upande wa Afisi ya Unguja.

Kujiunga na jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

111. Mheshimiwa Spika, Afisi tayari imeshaomba uanachama wa vyama vya Watunzi na Washairi ulimwenguni

(**Confederation of the Societies of Authors and Composers – CISAC)** baada ya kutimiza masharti ya kuwa na idadi maalum ya wanachama na inasubiri kujibiwa. Uanachama huu ndio utakaowezesha wasanii wa Zanzibar kutambulika na kupata haki na maslahi yao nje ya nchi kwa kuwa na uwezo wa kuingia mikataba ya kusimamia haki **(Bilateral Agreement)**

112. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2008/ 2009 Afisi imejipangia kutekeleza yafuatayo:-

I. Kuimarisha utendeji wa Afisi,
II. Kukuza uelewa wa jamii juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki Zanzibar; na
III. Kuendesha utafiti wa kuelewa kiwango cha ubunifu Zanzibar na mchango wake kwa uchumi wa taifa,

113. Mheshimiwa Spika, Ili Afisi iweze kumudu na kutekeleza vyema mipango na majukumu yake katika kipindi cha 2008/2009 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 120,000,000.00

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

114. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iliidhinishiwa Ruzuku ya Jumla ya Shilingi 115,661,303.00. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2008 fedha zilizopatikana ni Shilingi 89,505,673.00. Kati ya fedha hizo shilingi 86,323,515.00 zilitumika kwa kulipia mishahara na maposho na shillingi 3,182,158.00 kwa matumizi mengineyo. *(angalia kiambatisho namba 1)*. Kutokana na upatikanaji huo wa fedha, pamoja na kazi za kawaida katika kipindi cha Julai 2007 hadi Machi 2008, Kamisheni imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo: -

Kuandaa kanuni zitakazoiwezesha sheria namba 2 ya 2007 kuwa na ufanisi zaidi.

115. Mheshimiwa Spika, tayari rasimu tatu za kanuni zimeshaandaliwa, Rasimu za kanuni hizo ni Wasia na Mirathi, Hiba na Wakfu, na Malipo ya ada na huduma. Rasimu za kanuni hizo zinatarajiwa kupitishwa katika Bodi ya Kamisheni kabla ya kupelekwa/kuletwa wizarani kwa hatua za Waziri kuzitangaza.

Kuendeleza kazi za kuhifadhi kumbukumbu za Wakfu, Amana na Mirathi

116. Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhifadhi kumbukumbu za Wakfu na Amana imeshafanyika. Aidha Kamisheni kupitia kitengo cha shughuli za kiislamu ilifanya kazi ya kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu za misikiti na madrasa zote za Unguja.

Marekebisho ya mikataba ya nyumba na kuanzisha mikataba na kodi mpya.

117. Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na manung'uniko ya wanufaika wa Mali za Wakfu na Amana kuhusiana na viwango vidogo vya kodi wanazotozwa wapangaji wa nyumba hizo. Kufuatia utafiti uliofanywa na Kamisheni, imedhihirika kuwa viwango vya kodi vya nyumba za Wakfu na zile za Amana viko chini mno na haviendani na wakati na hali halisi ya soko. Kwa hali hiyo Kamisheni iliwaarifu wapangaji wake wote juu ya uamuzi wa kufutwa kwa mikataba yote ya nyumba na kuanza kutolewa mikataba mipya kuanzia tarehe 16/3/2008. Zoezi la ubadilishaji huo wa mikataba linaendelea vizuri.

Kufanya utafiti na kuweka utaratibu madhubuti wa ukusanyaji, uhifadhi na ugawaji wa Zakka.

118. Mheshimiwa Spika, Hatua ya mwanzo ya kufanikisha lengo hili ni kujua vikundi vyote vinavyoshughulika na kazi hii. Kwa mashirikiano na Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Kamisheni imeorodhesha vikundi vilivyosajiliwa na kujishughulisha na kazi hiyo. Aidha Kamisheni imewaita baadhi ya viongozi wa vikundi hivyo na kuwafahamisha juu ya jukumu la Kamisheni ya Wakfu kisheria katika masuala ya Zakka. Kamisheni pia inakusudia kutayarisha kanuni na kukutana tena na viongozi wa vikundi hivyo ili kushauriana zaidi namna ya kuimarisha usimamizi wa Zakka nchini.

119. Mheshimiwa Spika Kamisheni imekuwa ikishirikiana kwa karibu zaidi na Jumuiya na Taasisi mbali mbali za Kidini ndani na nje ya nchi. Jumla ya marobota 28 ya vitambaa yalipokelewa ikiwa ni msaada kutoka Dubai na kugawiwa katika vyuo mbali mbali vya Qur'an mjini na mashamba. Aidha Afisi ilipokea jumla ya misahafu 1000 kutoka Qatar na Katuni 1963 za tende kutoka Falme za Kiarabu na kugawiwa kwa waislamu Unguja na Pemba. Kamisheni pia imekuwa ikiziombea misamaha ya ushuru wa forodha Jumuiya mbali mbali za Kiislamu zilizopo hapa Zanzibar.

Kuimarisha utendaji wa kazi na kunyanyua hali za wafanyakazi.

120. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha utendaji wa kazi na kunyanyua hali za wafanyakazi, Kamisheni katika kipindi cha 2007/2008 imepeleka wafanyakazi wawili masomo ya muda mrefu katika ngazi za Stashahada ya Elimu na Shahada ya Pili

na watatu kwa mafunzo ya muda mfupi. (angalia kiambatisho namba 6a na b)

121. Mheshimiwa Spika, Pamoja na utekelezaji wa malengo Kamisheni ya Wakfu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida kama ifuatavyo:-

Hadi kufikia Machi 2008 Kamisheni imeendelea kusimamia nyumba 392 za Wakfu, nyumba 75 za Amana na vikataa 12 vya Wakfu na Amana kwa Unguja na Pemba. Aidha Kamisheni inaendelea na ujenzi wa nyumba mpya katika plot namba 202 huko Mbweni.

122. Mheshimiwa Spika, Kamisheni imekusanya jumla ya shilingi 95,905,900.00 ikiwa ni kodi kwa mali za Wakfu na shilingi 16,085,000.00 kwa mali za Amana hadi kufikia mwezi Machi 2008. Hii ni sawa na asilimia 90.05 ya lengo lililokusudiwa la kukusanya shilingi 124,353,599.85.00. Hata hivyo Kamisheni bado inaendelea kudai shilingi 18,800,000.00 kutoka Taasisi za kiserikali

123. Mheshimiwa Spika, Hadi mwishoni mwa Machi 2008 jumla ya tirka mpya 451 zimefunguliwa. Aidha tirka 615 zenye ushuru wa thamani ya Shilingi 44,805,579.00 zimefungwa baada ya kukamilika kurithishwa. Idadi ya tirka zinazoendelea kushughulikiwa ni 159.

124. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hijja, Mahujaji 1870 walikwenda kutekeleza ibada hiyo mwaka 2007/2008. (kwa Tanzania nzima). Idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 26.77 ukilinganisha na idadi ya mwaka jana. Mashirika ya Zanzibar kwa mwaka huu yalipeleka Mahujaji 1262 ikiwa ni asilimia 67.48 ya Mahujaji wote wa Tanzania. Orodha ya vikundi vya

Zanzibar vilivyosafirisha Mahujaji na gharama za kila kikundi zinaonekana katika kiambatanisho namba 10.

125. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imejiwekea malengo yafuatayo:-

I. Kuongeza uwezo na uelewa wa sheria ya Kamisheni kwa wadau wakuu wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;
II. Kuimarisha utendaji wa Kamisheni; na
III. Kuendeleza mapambano dhidi ya HIV/UKIMWI.

126. Mheshimiwa Spika, Ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kumudu na kutekeleza vyema mipango na majukumu yake katika kipindi cha 2008/2009 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 155,000,000.00

AFISI KUU PEMBA

127. Mheshimiwa Spika, Afisi kuu –Pemba imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za wizara na malengo iliyojipangia kwa ufanisi ikiwa ni kiungo kati ya taasisi za ndani ya wizara, nje ya wizara, baina ya wizara na sekta binafsi kwa upande wa Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 afisi imeratibu maombi ya jumuiya za kiraia 11 zilizopata usajili. Aidha kupitia afisi ya Naibu Mufti, afisi imeendelea kutoa fatwa, kusuluhisha migogoro ya wanandoa, kuitembelea misikiti na madrasa na kusisitiza suala la amani, utulivu na mashirikiano ndani ya jamii pamoja na kuhimiza kuwafundisha watoto malezi na tabia njema ili wawe raia wema wa baadae.

128. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008, Afisi kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya shilingi 284,208,000.00 ambapo shilingi 50,121,000.00 ni ruzuku kwa ajili ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba. Kati ya shillingi 168,890,600.00 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 115,317,400.00 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2008 fedha zilizopatikana ni shilingi 170,462,508.00 sawa na asilimia 60. Kati ya hizo shilingi 112,124,980.00 ni mishahara na maposho , sawa na asilimia 66.4, na shilingi 58,337,528.00 sawa na asilimia 51 kwa matumizi mangineyo. (*angalia kiambatiisho namba 1)*.

129. Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji huo wa fedha, pamoja na kazi za kawaida Afisi kuu Pemba ilitekeleza malengo yake kwa mwaka 2007/2008 kama ifuatavyo:

Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma.

130. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hichi wafanyakazi 3 wamemaliza masomo ya muda mrefu, mmoja Shahada ya kwanza katika fani ya sheria, Stashahada ya juu ya mipango na maendeleo ya rasilimali watu na mwengine cheti cha mafunzo ya utawala. Aidha wafanyakazi wengine kumi wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

Kuimarisha utendaji wa Afisi

131. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Afisi imeweza kuimarisha utendaji kwa mafanikio makubwa

ikiwa ni pamoja na kulifanyia matengenezo jengo la afisi, kupunguza tatizo la usafiri na vitendea kazi.

Kuendelea kutoa taaluma ya ukimwi kwa wafanyakazi

132. Mheshimiwa Spika, Afisi imeendelea kuwaelimisha wafanyakazi wake kwa kuzidi kujenga uelewa wa athari ya virusi vya UKIMWI. Aidha kwa msaada wa kifedha kutoka Tume ya ukimwi Zanzibar (ZAC) waelimishaji rika 10 wamepatiwa mafunzo ambapo wahusika baada ya mafunzo hayo wameanza kutoa taaluma hiyo katika taasisi zao.

133. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 Afisi kuu pamoja na kusimamia na kuratibu shughuli za Wizara imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

I. Kuimarisha uwezo wa Afisi katika kuratibu shughuli za kazi za Wizara Pemba,
II. Kuendelea na mpango wa kutoa taaluma ya elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi na familia zao

134. Mheshimiwa Spika, Ili afisi kuu Pemba iweze kutekeleza malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2008/2009 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 263,435,000.00.

SHUKURANI

135. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Wizara yangu nachukua fursa hii tena kuipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu kwa maelekezo na ushauri wao kwa Wizara. Aidha napenda kuishukuru Kamati ya Ahadi kwa kuendelea kuhakikisha tunatekeleza ahadi zetu

tulizozitoa. Pia natoa shukrani kwa Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Idara, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara kwa utendaji wao. Aidha kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya watendaji wa Wizara yangu nawashukuru wajumbe wako wote kwa michango yao yenye faida kwa Wizara yangu.

136. Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Visiwa hivi vya Unguja na Pemba kwa kuiunga mkono vizuri Wizara yangu katika utekelezaji wa majukumu yake na kukubali kufanya kazi nayo kwa kuipa mashirikiano inayostahiki. Ninaamini kwamba wananchi watazidi kuwa karibu na Wizara yangu kwa maslahi ya nchi yetu.

137. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na kuthamini mashirikiano ambayo imekuwa ikiyapata kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na wadau mbali mbali ndani na nje ya nchi na kwa heshima na taadhima naomba ruhusa yako kuwashukuru wale wote wanaotusaidia wakiwemo UNDP, ADB, WIPO, UNICEF, UNFPA, GLOBAL FUND na WORLD BANK, Serikali ya Oman, Islamic Development Bank, An-noor Charitable Society for the Needy, Al-Yousouf Charitable Society, Africa Muslims Agency, na Vikundi mbali mbali vilivyosafirisha mahujaji.

HITIMISHO

138. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yote hayo na ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake na malengo iliyojipangia, naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 ya jumla ya shilingi 4,648,450,000.00 kwa kazi za

kawaida na shilingi 720,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha naliomba Baraza lako likubali mchango wa shilingi 292,928,000.00 ikiwa ni mapato yatakayokusanywa na Wizara hii ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali *(angalia viambatisho 2 na 4)*.

139. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

RAMADHAN ABDALLA SHAABANI
WAZIRI WA NCHI (AR)
KATIBA NA UTAWALA BORA
ZANZIBAR

KIAMBATISHO NAMBA 12 MISWAADA YA SHERIA KWA MWAKA 2007/2008

I. Mswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2007/2008;
II. Mswada wa Sheria ya Fedha, Usimamizi na Mapato ya Serikali - 2007.
III. Mswada wa Sheria ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali – 2007.
IV. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Uhaulishaji Ardhi - 2007.
V. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria za Mafunzo ya Amali - 2007.
VI. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar – 2008.
VII. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mahkama ya Ardhi - 2008.
VIII. Mswada wa Sheria ya kuanzisha Idara ya Makumbusho na Kumbukumbu - 2008.
IX. Mswada wa Sheria ya Tasnia ya Mali za Ubunifu na Hataza - 2008.
X. Mswada wa Sheria ya Tiba Asilia na Tiba Mbadala - 2008.
XI. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi za Wakandarasi – 2008.
XII. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Wahandisi, Wasanifu na Wakadiriaji Majenzi.
XIII. Mswada wa Sheria ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii - 2008.

Aidha, Afisi iliweza kutayarisha Sheria ndogo ndogo na Kanuni (Subsidiary Legislations) 12. Miongoni mwao zikiwa ni :-

I. Kanuni za Kuliendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; -2007
II. Kanuni kuhusu Bodi ya Upimaji wa Ardhi; - 2007
III. Kanuni za Usajili na Utoaji wa Leseni za Vyombo vya Moto; -2007
IV. Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar; -2007
V. Kanuni kuhusu Usafiri wa Baharini; - 2007
VI. Kanuni za Mahkama za Rufaa ya Idara Maalum za SMZ -2008
VII. Kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ - 2008
VIII. Kanuni za Usajili wa Mabaharia - 2008